**SHULE YA SEKONDARI TONGANI**

**(Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule)**


**Sim: 0629 147 349** **S.L.P 05,**

**0627 637 204** **PANGANI,**


**Tarehe……………..**

---

**Namba za simu**

Mkuu wa shule 0629 147 349

Makamu Mkuu wa Shule 0627 637 204

Matroni 0625 188 084

Mwalimu mwandamizi Taaluma 0716787349

Mzazi/ Mlezi wa

…………………………………………………

S. L.P………………………...

…………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI TONGANI HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI MKOA WA TANGA MWAKA………………..**

1. **UTANGULIZI**
   Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka…………………….tahasusi ya PCB/CBG (kata isiyohusika)

   Shule ya Sekondari Tongani ni shule ya **mchanganyiko** kwa kidato **I-IV** na ni ya **wavulana** kwa kidato **V-VI** (mchepuo wa sayansi-**PCB** na **CBG**) na ipo umbali wa kilometa **75** kusini mwa makao makuu ya wilaya ya Pangani.

2. **NAMNA YA KUFIKA SHULENI**
   Unaweza kufika shuleni kupitia mojawapo ya njia zifuatazo:-
   - Ukitokea Tanga mjini; panda basi la moja kwa moja liitwalo Makata ya kuelekea mkalamo nauli sh. 9000 (muhimu kuwahi asubuhi kabla ya saa nne gari ipo moja tu) **AU** panda gari mpaka ukifika Pangani mjini vuka kivuko (nauli sh.200) utafika mji mdogo unaoitwa Bweni. Uliza mabasi yanayokwenda Mkalamo (Kidato, Makata, Passion na Sharifa nauli sh. 6000) waambie wakushushe Tongani Sekondari.
   - Ukitokea Dar es Salaam; panda basi la Passion au Sharifa (Stand ya Magomeni Kagera nauli sh. **18,000/=** waambie wakushushe Tongani Sekondari au panda treni (siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa) shukia stesheni ya mkalamo.

- Ukitokea mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Dar es Salaam na kwingineko shuka mji mdogo wa **Mkata** (njia panda ya kwenda Handeni) uliza mabasi ya kwenda Mkalamo-Pangani (Kidato, Passion au sharifa nauli sh. 7000/= waambie wakushushe Tongani Sekondari au panda treni (siku ya Jumanne, Alhamisi na Jumamosi) shukia stesheni ya mkalamo.
- **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu kwa kisingizio chochote kiwe cha umbali au sababu nyingine hivyo kama hawezi kufika mwenyewe aletwe na mzazi au mlezi wake lakini ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na simu shuleni.**

## 3. MUHULA WA MASOMO

Muhula wa masomo unaanza tarehe**……………**Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………………….na sio zaidi ya tarehe…………………**.**

## 4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 4.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni suruali ya khaki yenye malinda na upana wa sentimita 17 (asiyefuata maagizo haya hatapokelewa), shati nyeupe ya mikono mafupi.
b) Tai **special** rangi ya khaki, ukipenda zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh elfu kumi (10,000/=).
c) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
d) Soksi jozi mbili nyeupe
e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
f) Sweta rangi ya dark blue (kama utahitaji kuvaa japokuwa Pangani kuna joto kali).



*Figure 2 Sweta la shule*



*Figure 1Suruali ya shule*

g) Nguo za michezo ni track-suit rangi ya dark blue, bukta ya dark blue na fulana (t-shirt) rangi ya dark bue (t-shirt isiwe na maandishi).




h) Mwanafunzi anatakiwa kuja na raba za michezo hizi zitatumika wakati wa jogging pia kwa mchezaji mpira wa miguu aje na viatu vyenye meno maalumu kwa ajili ya kuchezea mpira.

i) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali za kijani na T-shirt za dark blue (T-shirt zinaweza kupatikana shuleni kwa sh **15,000/= ukipenda**).

**4.2 Michango mingine**

a) Fedha zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. **42001200039** katika benki ya **NMB** jina la A/C **Tongani Secondary School** (tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye benki pay-in-slip na aje nayo shuleni nakala halisi siku anaporipoti)

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

| **Aina ya mchango** | **Kiasi** |
|---|---|
| Mchango wa uendeshaji shule | 65,000/= |
| Tahadhari | 5,000/= |
| Nembo | 5,000/= |
| Kitambulisho Cha shule | 5,000/= |
| Jumla | 80,000/= |

***Ada na michango yote ilipwe kwenye Akaunti ya Shule*** **42001200039** benki ya **NMB** jina la A/C **Tongani Secondary School.**

**4.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

(i) Ream ya karatasi A4 (bundle mbili (02) kwa mwaka) kabidhi ofisini wakati anaripoti.
(ii) Dissecting kit-01(kabidhi ofisini wakata anaripoti).
(iii) Scientific calculator 1 (fx 991)- (itakaguliwa ofisini wakata anaripoti).
(iv) Godoro futi 2 1/2 upana na urefu futi 6
(v) Mashuka mawili ya rangi ya light blue
(vi) Mto mmoja wenye foronya ya rangi ya light blue
(vii) Chandarua 1 (rangi ya bluu).
(viii) Taulo ya kuogea
(ix) Vyombo vya kulia chakula Container na kijiko.
(x) Jembe (1) (PCB na CBG), Soft broom (1) (CBG), kwanja (1) (CBG), kisugua sink cha mbao (scrubber) (1) (PCB) na panga (1) (PCB).
(xi) Ndoo ndogo 2 (moja utaikabidhi shuleni na moja ni kwa matumizi yako ya usafi),
(xii) Dissecting tray 1- (kabidhi ofisini wakata anaripoti).
(xiii) Graph pad 1 (kwa matumizi yake)
(xiv) Ndala za kuogea (rangi ya bluu).
(xv) Blancket kwa mwenye uhitaji japokuwa hali ya hewa ni joto. **Hairuhusiwi kuja na shuka la kimasai.**
(xvi) Folder file kwa ajili ya kuhifadhia mitihani.

***Faili la kuhifadhia mitihani na nyaraka muhimu kama vyeti.***



**TANBIHI:**

1. Kwa matumizi binafsi mwanafunzi anashauriwa kujinunulia walau nakala moja ya kitabu kwa kila somo kulingana na tahasusi yake na vitakaguliwa siku anaripoti shuleni. orodha ya vitabu kwa kila somo imeambatanishwa.
2. Siku ya kuripoti aje na nakala (copy) ya **result slip** na **Cheti cha kuzaliwa, Tafadhali usije na vyeti original.**
3. Kwa mwanafunzi mwenye bima ya afya aje nayo kwa ajili ya matibabu yake pindi anapopanda changamoto ya kiafya.

## 5. KANUNI ZA SHULE

1. Mwanafunzi atavaa sare rasmi za shule anapokuja kuripoti shule, akiwa shuleni na anaporudi nyumbani kipindi cha likizo.**Hairuhusiwi kuvaa mavazi tofauti na sare za shule.**
2. Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isispokuwa anapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu,Makamu mkuu wa shule au mkuu wa shule.
3. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare rasmi za shule muda wote wa shule, isipokuwa muda wa kazi za mikono atavaa shamba dress na wakati wa michezo atavaa nguo za michezo.
4. Ni marufuku mwanafunzi kutumia lugha chafu, matusi,kupigana na fitina.
5. Mwanafunzi lazima awahi mahali anapotakiwa na kwa muda uliowekwa.
6. Mwanafunzi ni lazima aheshimu kazi za darasani ana kazi za nje, ni lazima kufanya mazoezi yote yanayotolewa na walimu darasani.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia kileo chocote wala kuvuta sigara,bangi au madawa yoyote ya kulevya.
8. Ni marufuku kuiba au kushirikiana na mwizi kwa njia yoyote ile.
9. Ni marufuku kuharibu au kupoteza mali yoyote ya umma au binafsi.
10. Mwanafunzi anapaswa kuwa na heshima,mtiifu na nidhamu wakati wote.
11. Mgeni wa mwanafunzi ataruhusiwa kuonana na mwanafunzi baada ya kupokelewa na kujitambulisha na mwalimu wa zamu. (mwanafunzi anaruhusiwa kutembelewa jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa sita mchana hadi saa kumi kamili jioni).
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuwa na mahusiano yoyote ya kimapenzi.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda katika nyumba za walimu bila ruhusa maalumu ya mwalimu mlezi au uongozi wa shule.
14. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote, hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mbalimbali.(Aidha mikanda mipana ,cheni, herein,vipochi,mikufu,pete,miwani ya urembo,shanga za mikononi,kofia, mashuka ya kimasai na majaketi ni marufuku kabisa shuleni).
15. Hairuhusiwi kuja na simu, kukutwa na simu au kifaa chochote cha mawasiliano ukikamatwa **utapewa adhabu kali na kulipa fidia za uharibifu wa miundombinu ya umeme.**
16. Ni marufuk mwanafunzi kugomea/kukataa adhabu kwani kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako shuleni.
17. Mwanafunzi haruhusiwi kugoma au kuhamasisha mgomo,**yeyote atakaebainika kugoma au kuhamasisha mgomo atafukuzwa shule**.
18. Lazima wanafunzi kuheshimu na kuwatii viranja, walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi wengine

## 6. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi wa mali za umma na mali binafsi.

2. Utoro (kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa)

3. Uasherati, ushoga na ubakaji.
4. ‘
5. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

6. kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

7. Kupiga au kupigana

8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma kama vile samani za shule (viti,meza,vitanda nk) kwa makusudi.

9. Kudharau wimbo wa Taifa, wimbo wa shule na bendera ya Taifa.

10. Kuoa au Kuolewa.

11. Kusababisha mimba.

12. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa jumaiya ya shule.

13. Kukataa adhabu kwa makusudi

14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi, line ya simu au kifaa chochote cha mawasiliano katika mazingira ya shule.
15. Hairuhusiwi kumiliki pasi ya aina yoyote katika mazingira ya shule.
16. Kunyanyapaa au kufanya uonevu wa aina yoyote kwa mwanafuunzi mwingine.

7. **MWISHO**:

Hakikisha unafika shuleni tarehe iliyopangwa. Usipo fanya hivyo, wala kutoa taarifa ya kutofika utahesabiwa kuwa hutafika na nafasi itarudishwa katika mamlaka husika za uchaguzi ili nafasi hiyo wazi iweze kuchukuliwa na mwanafunzi mwengine. Mzazi/mlezi una wajibu wa kumpatia mwanao **fedha za kujikimu** awapo shuleni pamoja na **nauli** ya kwenda na kurudi wakati wa likizo au kwa dharura yoyote.
Ninachukua nafasi hii kukukaribisha tena Tongani Sekondari na ni matarajio yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako.

Karibu sana.

……………………
SAIMON P. LUFUNGA
**(*mkuu wa shule)***

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI TONGANI**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

| PICHA |
|---|
| |

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:
JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………
TAREHE YA KUZALIWA ……………………………………………………………
MAHALI ALIPO ZALIWA (MKOA/WILAYA) ……………………………………………
MNAISHI/MNAKAA WAPI (KATA/MTAA) ………………………………………………
URAIA ……………………………………………….
SHULE ALIYOTOKA ………………………………………….
NAMBA YA MTIHANI ………………………………………

B: TAARIFA YA MZAZI:
JINA LA MZAZI/MLEZI
……………………………………………………………………………………….
KAZI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………
ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………..
SIMU YA MZAZI/MLEZI: KAZINI ………………………………………………...
NYUMBANI …………………………………… MKONONI ……..……………………..

**C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA:**
Mimi ………………………………………………………. Kidato ………………… mwaka ……………..
Nimesoma na nakuayaelewa yote. Kwa hiyo nakubalia kuipokea /sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa na nitayazingatia.
Tarehe …………………………………… Sahihi ………………

**D: KUKUBALI SHERIAZASHULE:/ MWANAFUNZI.**
Mimi ………………………………………………………………. Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayo pewa na walimu wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwedhidi yangu kwa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.
Tarehe ………………………………………….. Sahihi ……………

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA/MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

E: MAZAZI/ MLEZI – (ajaze sehemu hii)

i. Mimi ………………………………………………….ambaye ni Mzazi/mlezi, nathibitisha kuwa mwanangu ……………………………………………jina la (mtoto)ameelewa maagizo ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanagu ni ……………………………… dhehebu lake ni ……………………………………………

ii. Ninaruhusu/siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje na ndani ya mkoa wa Tanga zitakazo fanyika kwa ruhusa ya mkuu wa shule hii.

iii. Nimeruhusu/ siruhusu (kata isiyohusika) wakati w a likizo fupi (mid term) mwanangu atoke shuleni na kwenda kwa …………………………………………… wa (mahali) ……………………………………………….. uhusiano wake na mwanangu ni ………………………………………………………….. namba yake ya simu ni ………………………………………………………..

iv. Aidha
mimi ……………………….…………….. ambaye ni mzazi/mlezi,nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayohusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi) ………………………………………………………naahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi/mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

(v) picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

| JINA LA MZAZI /MLEZI | NDUGU 1 | NDUGU 2 | NDUGU 3 |
|---|---|---|---|
| …………………………….. | ………………………. | ………………………. | ……………. |
| SIMU……………………….. | ………………………. | ………………………. | ……………… |
| UHUSIANO…………………… | ……………………….. | ……………… | …..……………. |

…………………………… …………………………..

JINA LA MZAZI/MLEZI SAHIHI

TAREHE……………………………

**THE PRIME MINISTER'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A

The Headmaster,
Tongani Secondary School,
P. o. Box 05,
Pangani – Tanga.

TO,
The Medical office,
……………………………
……………………………
…………………………….
………………………………………………………. (Name of student in full) please examine the above-mentioned student as to her physical and mental fitness for a full-time student. The examination should include the following category (a- c)

a. (i). Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease

(v) Limbs

b. Neurosis

c. Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc

Name …………………………… Date ……………………...signature …………………
PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(to be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that she is fit/unfit full-time studies.

i. Eyesight ………………………………………………….

ii. Hearing ……………………………………………………

iii. Speech ……………………………………………………..

iv. Limbs ………………………………………………………

v. Venereal diseases …………………………………………….

vi. Leprosy ……………………………………………………….

vii. Epilepsy ……………………………………………………

viii. Neurosis ……………………………………………………

ix. Other serious diseases eg. Asthma ……………………………………..

x. Allege reaction of some drugs …………………………………………………

xi. T.B …………………………………………………………….

Other Comments ……………………………………………………………………
Name ……………………………… Date ………………… Signature ……………………
STATION ………………………………….. DESIGNATION ……………………………..
**Official stamp**……………………………………..

**PREFERENCES OF STUDENTS TEXT BOOKS A-LEVEL**

| SUBJECT | BOOKS |
|---|---|
| BIOLOGY | 1. Biological science, 3rd edition, Cambridge U.K, Taylor D.J et all (1997).<br>2. Understanding Biology for Advanced Level, 4th edition, Stanley Thorns L.t.d Uk, Glenn $ Suzan (1999)<br>3. Human Biology, 7th edition. Mcgraw hill companies, New York, Sylivia Mader (2002). |
| CHEMISTRY | 1. Tanzania Institute of Education, (1995) "General and Inorganic Chemistry." Dar es Salaam Un. Press. (Revised 2024).<br>2. Tanzania Institute of Education 'Physical chemistry for Advanced secondary schools. (Revised 2024)<br>3. Tanzania Institute of Education, (1995) "Organic Chemistry." Dar es Salaam Un. Press. (Revised 2024). |
| PHYSICS | 1. ABC MORDEN PHYSICS: (VOLUME I & II.<br>2. ROGER MUNCASTER – PHYSICS.<br>3. TOM DUNCAN – PHYSICS.<br>4. CHAND'S – PHYSICS (CLASS XI & XII). |
| BAM | 1. Tanzania institute of Ed (2019), Basic Applied Mathematics for Advanced level Secondary Education form V and VI. Dar es Salaam Ministry of Education and Vocation Training.<br>2. Basic Applied Mathematics Review – (Necta). |
| GEOGRAPHY | 1. Bunnet, R.B (1984) Physical Geographycial in diagrams for a Africa Longman Group Limited. England.<br>2. Pritchard. J.M. (1990) Practical Geography for Africa. Longman Group L.td Hong Kong.<br>3. Tanzania Institute of Education (2016) Geography for Secondary form five Tanzania.<br>4. Msabila, D.T (2003) An Integrated focal Reginal study on Human and Economic Geography. Nyambari Nyangwine Publisher Dar es Salaam. |
| HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | 1. Historia ya Tanzania na Maadili form V (TIE). |
| ACADEMIC COMMUNICATION | 1. Academic Communication form V-(TIE). |